

69

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Anwani ya Simu: "ELIMU"
DAR ES SALAAM
SIMU: 2110146, 211050/2, 2110179
Telex: 41742 Elimu Tz
Fax: +255-22-2113271



7 MTAALI WA MAGOGONI,
11479 DAR ES SALAAM.

Kumb. Na: ED/OKE/NE/Vol.1/01/43

Tarehe: 7/08/2014

Katibu Mkuu, OWM-TAMISEMI,
Mwenyekiti - TAMONGSCO,

**WARAKA WA ELIMU NA. 4 WA MWAKA 2014 KUHUSU UTAYARISHAJI
WA VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA KUFUNDISHIA**

1. UTANGULIZI

Kabla ya mwaka 1991, jukumu la kuandika vitabu liliwa la Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ambapo kitabu kimoja cha kiada kilitumika kwa kila somo kwa shule zote Tanzania Bara.

Mwaka 1991 Wizara ilipitisha utaratibu mpya wa Uzalishaji na Usambazaji wa Vitabu Shuleni na Vyuo vya Ualimu. Utaratibu mpya pamoja na mambo mengine uliweka mfumo huria wa uzalishaji na usambazaji wa vitabu na vifaa vingine vya kielimu nchini na ulielekeza Wizara ya Elimu kujitoa katika uandishi wa vitabu na kuacha jukumu hilo kwa wachapishaji binafsi. Aidha utaratibu mpya ulielekeza matumizi ya kitabu cha kiada zaidi ya kimoja kwa kila somo kwa kila darasa.

Ili kutekeleza utaratibu huo Waraka wa Elimu Na 2 wa mwaka 1998 ultolewa ambapo Kitengo cha Usimamizi wa Machapisho na Vifaa vya Kielimu (BMU- Book Management Unit) kilianzishwa. Kuokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza, waraka huo ulifutwa mwaka 2005 kwa Waraka wa Elimu Na. 7 ulioanzisha Kamati ya Ithibati ya Vifaa vya kielimu nchini (EMAC - Educational Materials Approval Committee).

2. HALI HALISI YA UTEKELEZAJI


Pamoja na kutolewa kwa Waraka wa Elimu Na. 7 wa mwaka 2005, bado changamoto za ubora wa vitabu na vifaa vingine vya kielimu ziliendelea kujitokeza na hivyo kuathiri ubora wa elimu. Aidha, mwaka 2009, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliagiza matumizi ya kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo na kwa kila darasa nchi nzima. Ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza na

kutekeleza agizo hilo ilifanyika tathmini na mchakato wa marekebisho ya mfumo mzima wa uandaaji na utoaji wa ithibati wa vitabu na vifaa vingine vya kielimu.

Kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hiyo na marekebisho ya mfumo huo Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Usundi kwa mamlaka aliyonayo chini ya "Kifungu Na 5 cha Sheria ya Elimu Sura ya 353" amefuta Sera ya Uzalishaji na Usambazaji wa Vitabu Shulen na Vyuo vya Ualimu ya Mwaka 1991 pia amefuta Waraka wa Elimu Na. 7 wa mwaka 2005. Aidha, utaratibu mpya wa uandaaji na utoaji ithibati wa vitabu na vifaa vingine vya kielimu chini ya Taasisi ya Elimu Tanzania umeainishwa katika mwongozo ulioambatanishwa. Katika waraka huu.

Kufuatia mabadiliko hayo, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) itaandika na kuchapisha vitabu vya kiada (kitabu kimoja kwa kila darasa na kila somo) kwa ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu. Pia itaratibu maandalizi na uzalishaji wa vitabu vya ziada (reference books) na vifaa vingine vya kielimu (vifaa vya kujifunzia na kufundishia) vitakavyoandaliwa na wachapaji binafsi. (Utekelezaji wa jukumu hili umeainishwa katika mwongozo ulioambatanishwa na Waraka huu).

Waraka huu unafuta Waraka Na. 7 wa mwaka 2005, na unaanza, kutumika kuanzia tarehe 1/9/2014.



Prof. Eustella P. Bhalalusesa
KAMISHNA WA ELIMU

Nakala: Makatibu Tawala (M)/(W),
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya/Mji/ Manispaa/ Jiji,
Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),
Wakaguzi Wakuu wa Shule Kanda/Wilaya.